N10/2/ABSWA/SP1/SWA/TZ0/XX/T

88102391

International Baccalaureate®
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

**SWAHILI B – STANDARD LEVEL – PAPER 1**
**SOUAHÉLI B – NIVEAU MOYEN – ÉPREUVE 1**
**SUAHILI B – NIVEL MEDIO – PRUEBA 1**

Tuesday 2 November 2010 (morning)
Mardi 2 novembre 2010 (matin)
Martes 2 de noviembre de 2010 (mañana)

1 h 30 m

---

TEXT BOOKLET – INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this booklet until instructed to do so.
- This booklet contains all of the texts required for Paper 1.
- Answer the questions in the Question and Answer Booklet provided.

LIVRET DE TEXTES – INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- N'ouvrez pas ce livret avant d'y être autorisé(e).
- Ce livret contient tous les textes nécessaires à l'Épreuve 1.
- Répondez à toutes les questions dans le livret de questions et réponses fourni.

CUADERNO DE TEXTOS – INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra este cuaderno hasta que se lo autoricen.
- Este cuaderno contiene todos los textos para la Prueba 1.
- Conteste todas las preguntas en el cuaderno de preguntas y respuestas.


© International Baccalaureate Organization 2010

https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU A**

# VYAKULA MBALIMBALI KATIKA AFRIKA YA MASHARIKI

*Lila na Fatuma ni marafiki wawili wanaosoma katika chuo cha uhasibu jijini Nairobi. Wanatafuta mahali pa kula chakula cha mchana wakisubiri madarasa yao.*

**Lila**: Mwenzangu sina nguvu za kutembea hadi bwenini kula.

**Fatuma**: Haya basi tutafute mahali pa kwenda tule haraka kisha turudi darasani.

**Lila**: Twende tuujaribu ule mkahawa wa Baraka na Mama Aisha!

**Fatuma**: Ninafikiri ni bora Mama Aisha, hawapiki nyama ya nguruwe. Twende.

**Mhudumu wa Hoteli**: Karibuni. Kuna nafasi pale kwenye meza ndogo ya pembeni.

**Fatuma**: Asante.

**Mhudumu wa Hoteli**: Je, mngetaka kula nini leo?

**Lila**: Tutahitaji menu yenu kwanza.

**Mhudumu wa Hoteli**: Oh! Samahani sana. Ndiyo hii hapa.

**Fatuma**: Asante, tutakuita tukiwa tayari.

**Lila**: Mbona sioni ninachokihitaji?

**Fatuma**: Ulikuwa unatafuta chakula cha aina gani? Hiba aliniambia ya kwamba hapa wana maini, wali na sambusa nzuri.

**Lila**: Oh! Zimeorodheshwa katika ukurasa wa pili wa menu. Mimi nitajaribu viazi vilivyokaangwa, mchuzi wa uyoga na maji ya matunda ya mapera.

**Fatuma**: Ninaona kweli ulikuwa na njaa. Hebu nione. Ninafikiri nitakula samaki na wali wa kukaangwa. Pia nitakunywa maji ya matunda ya karakara.

**Lila**: Tahadhari na vitu vya mafuta mengi. Vinaweza kukuletea ugonjwa.

**Fatuma**: Ni mara moja tu lakini nitajitunza.

**Mhudumu wa Hoteli**: Aha! Je, mko tayari kuagiza mnachokitaka kula?

**Lila**: Naam! Ninafikiri nitajaribu viazi vya kukaangwa, mchuzi wa uyoga na maji ya mapera.

**Mhudumu wa Hoteli**: Viazi hivyo utataka viandamane na nini? Kuna kuku, nyama ya mbuzi, nyama ya kondoo na nyama ya ng'ombe.

**Lila**: Nipe nyama ya mbuzi tafadhali.

**Mhudumu wa Hoteli**: Sawa. Na wewe dada?

**Fatuma**: Mimi ninataka uniletee wali na samaki wa kukaangwa. Je, mna samaki gani?

**Mhudumu wa Hoteli**: Hapa tunapika samaki aina ya tilapia.

**Fatuma**: Sawa basi.

**Mhudumu wa Hoteli**: Utakunywa chochote?

**Lila**: Naam. Tafadhali niletee maji ya matunda ya mapera.

**Mhudumu wa Hoteli**: Usijali dada, nitafanya hivyo.


L Muaka, *et al.*, (2006), *Tusome Kiswahili*, NARLC, Publishers, Wisconsin-Madison



https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU B**

# JIJI LA NAIROBI



❶ Nairobi ndio jiji kubwa nchini Kenya. Ni jiji ambalo lina takriban watu milioni tatu. Jiji la Nairobi ni makao makuu ya mkoa wa Nairobi na pia makao maalum ya ofisi zote za serikali. Jiji limegawika katika sehemu nne za makazi. Kuna sehemu ya mashariki ambayo ndiyo makazi ya watu wa tabaka la chini, sehemu ya kusini ya mji ina watu wengi wa tabaka la kati. Magharibi mwa jiji la Nairobi ndiko kunakokaa matajiri wengi ingawa pia kuna sehemu za watu maskini. Sehemu za kaskazini kuna mchanganyiko wa watu maskini na wale tabaka la kati. Jiji la Nairobi linahudumiwa na uwanja wa ndege wa kimatifa wa Jomo Kenyatta na uwanja mdogo wa Wilson.

❷ Kwa sababu jiji la Nairobi ni la kimataifa, kuna watu kutoka nchi mbalimbali za ulimwengu. Pia, kuna ofisi nyingi za kimataifa kama vile za umoja wa mataifa, na makao makuu ya mradi wa mazingira wa kimataifa, UNEP. Wizara zote zina makao makuu jijini na bunge la nchi liko katika jiji hili. Pia, kuna ikulu ya rais na kaburi la rais wa kwanza wa nchi ya Kenya Mzee Jomo Kenyatta lipo karibu na majengo ya bunge. Jiji hili lina mahoteli na majumba ya mikutano makubwa ambako mikutano mingi ya kimataifa hufanyika. Jiji hili pia lipo katika sehemu nzuri katika eneo la Afrika ya Mashariki na ya Kati na ni pahali pazuri pa kuwaunganisha watu kutoka nchi mbalimbali.

❸ Kwa wale wanaopenda kustarehe, jiji la Nairobi lina sehemu nyingi za burudani. Kwa wale wanaopenda mambo ya utamaduni kuna huduma zinazoendeshwa na serikali kupitia idara ya "Bomas of Kenya", jumba la makumbusho la Nairobi, mbuga ya wanyama ya Nairobi, viwanja vya kuchezea na vidimbwi vingi vya kuogelea. Pia, kuna sehemu nyingi za kustarehe na kucheza ngoma wakati wa wikendi.

❹ Kwa upande wa usafiri kuna matatu chungu nzima na mabasi. Kuna pia huduma za gari la moshi na mabasi ya kwenda nje ya jiji na nchi nyingine. Kwa kweli ingawa kuna idadi kubwa ya watu, kuwepo kwa matatu nyingi kumepunguza shida za usafiri.

❺ Ingawa Nairobi ni jiji kubwa sana, kuna watu wengi wanaokuja katika jiji hili kutoka sehemu za mashambani kuuza mazao yao kama mboga, viazi, mahindi, maharagwe, mihogo, na kadhalika. Watu hawa huja kununua vifaa vya ukulima kama majembe, mbolea na mbegu. Wale ambao hawatoki mbali sana na jiji la Nairobi huja na kurudi kwao kila siku. Watu kama hawa ni wale wanaotoka mkoa wa kati, mkoa wa mashariki na baadhi ya sehemu za mkoa wa Bonde la Ufa zilizoko karibu na Nairobi.

L Muaka, *et al.*, (2006), *Tusome Kiswahili*, NARLC, Publishers, Wisconsin-Madison



https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU C**

# MALARIA KATIKA SEHEMU ZA KWETU



Jina langu ni Amina. Nilizaliwa Arusha Tanzania lakini jamaa zangu wengine wanaishi Dar es Salaam na wengine mjini Mombasa, Kenya. Mara kwa mara mimi huwatembelea jamaa zangu Mombasa kwa sababu ninapenda maisha ya huko na hali ya hewa ni nzuri pia.

Ingawa ninaipenda miji hiyo miwili, tatizo kubwa katika miji hiyo ni mbu ambao wanauma na kuufanya mwili wangu uwe na alama nyingi kwa sababu ya kujikuna. Shangazi yangu Rita wa Mombasa hunishauri nijipake mafuta ya kuwafukuza mbu. Usiku yeye hupuliza dawa ya mbu ya Super Doom na pia hunihimiza nitumie chandarua.

Ninapowatembelea binamu zangu mjini Dar, pia wao hunikumbusha kutumia chandarua ili nisiumwe. Tunapokaa nje jioni kubarizi hutubidi kujikinga dhidi ya mbu ambao ni hatari sana kwa sababu wanaweza kusababisha ugonjwa wa malaria na vifo. Kwa hivyo sisi huwasha mshumaa au hujipaka mafuta ya kuwafukuza mbu.

Daktari wetu mjini Arusha anaitwa Dkt. Otieno na anaelewa sana magonjwa ya sehemu hizi za Afrika ya Mashariki. Dkt. Otieno alizaliwa na kusomea nchini Kenya lakini alihamia Arusha kuanzisha zahanati yake ya utabibu. Kila mara Dkt. Otieno hutuhimiza kumeza tembe za kinga ya malaria kabla ya kusafiri sehemu za malaria kama vile pwani, sehemu za ziwa Victoria na kanda za juu kama Kisii na Kericho huko Kenya. Pia, daktari hutuambia tuishi katika mazingira safi ambayo hayawafichi mbu hatari. Yeye hupendekeza kumeza dawa za kujikinga dhidi ya malaria wiki mbili kabla ya kusafiri na wiki mbili baada ya kufika sehemu za malaria. Hushauri kuwa matibabu ya Malaria yakizidi ni bora kumwona daktari.

Kuna sababu nyingi za kuweko kwa mbu wanaosababisha magonjwa ya Malaria kwa mfano: vidimbwi vilivyojaa maji machafu kwa siku nyingi and nyasi zizizokatwa. Ili kuzuia ukuaji wa mbu ni bora kuondoa vianzo vyake, kuweka mazingira safi na kutumia dawa. Asimilia kubwa ya watu wengi barani Afrika huaga dunia kila kukicha kwa sababu ya ugonjwa wa Malaria kwa hivyo ni muhimu kufanya bidii zaidi ya mchwa kuuzuia ugonjwa huu. Shirika la kimatifa la Afya linafanya kampeni nyingi za kuangamiza Malaria.

K Njogu, *et al.*, (2003), Tanzu za Lugha, Jomo Kenyatta Publishers



https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU D**



# MISIMU MBALIMBALI KATIKA SEHEMU ZA AFRIKA YA MASHARIKI

Sehemu za Afrika ya Mashariki zina aina mbalimbali za misimu. Hata hivyo kuna baadhi ya sehemu ambazo misimu yake inaweza kujumuishwa. Hali ya anga huko inaathiriwa zaidi na hali zinazoendelea katika Bahari Hindi. Kwa upande mwingine hali anga kwenye sehemu za bara za Afrika ya Mashariki inaathiriwa pia na milima, mimea na masafa ya bahari.

Katika sehemu za Kenya mvua ya masika huanza mwezi wa tatu hadi mwezi wa tano au wa sita. Wakati huu mvua huwa nyingi na watu wengi ambao ni wakulima huyashughulikia mashamba yao. Baadhi ya mazao ambayo watu hupanda wakati huu ni mahindi, maharagwe na mboga. Baadhi ya mazao haya huchukua kati ya miezi miwili na miezi sita kukomaa.

Majira ya mvua fupi huja mwezi wa tisa hadi katikati mwa mwezi wa kumi na mbili. Wakati huu wakulima wachache hupanda mimea yao wakitegemea maji ya mvua. Kwa sababu viwango vya mvua huwa vidogo, mazao yanayopandwa ni yale ambayo huchukua muda mfupi kuwa tayari. Msimu wa kiangazi ni kati ya mwezi wa kumi na mbili na mwanzo wa wa mwezi wa tatu. Wakati huu wakulima wengi huyatayarisha mashamba yao. Huu ni wakati wa jua kali.

Afrika ya Mashariki haina theluji na baridi kali kama nchi za ng'ambo isipokuwa katika vilele vya milima Kenya na Kilimanjaro. Kwa sababu ni wenyeji wachache wanaokwea milima hii, ni watu wachache kutoka sehemu hizi ambao wana tajiriba ya theluji na baridi kali. Sehemu za nyanda, huwa na viwango vya joto vya kadiri mchana lakini usiku viwango vya baridi huongezeka. Baridi hii si kali sana kama ya nchi za ng'ambo. Kati ya mwezi wa sita na mwezi wa nane ni msimu wa kipupwe. Wakati huu ni wa baridi kidogo.

Ingawa sehemu nyingi za Afrika ya Mashariki hazina shida kama za ulimwengu uliondelea, taarifa kuhusu utabiri wa hali ya hewa ni muhimu kwa umma. Hii ni kwa sababu sehemu hizi zina ukulima ambao unategemea maji ya mvua na wakulima hutaka kuhakikisha kwamba wanapanda mazao yao wakati unaofaa kwa sababu wakichelewa huwa shida kupata maji ya kutosha. Kwa upande mwingine hawapaswi kupanda mimea yao kabla ya mvua kuja kwa sababu inaweza kuliwa na wadudu ardhini. Isitoshe, majira ya mvua yanaweza kuleta madhara kwa vitu na umma. Tofauti na nchi za ng'ambo, Afrika ya Mashariki haina vimbunga na tufani.

Taifa Leo (2008)



https://xtremepape.rs/